Mti Huu ni Mti Gani?

Cesilia Kunde

i

21st Century Basic Education Program(TZ21)
P. O. Box 34618
Dar es salaam

© Cesilia Kunde,2015

Mchoraji: Abdul Gugu
Usanifu: Sisi Illustrators

ISBN 978 9987 9448 9 7

Kitabu hiki kimechapishwa na TZ21 kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Misaada la Marekani (USAID) na kuwezeshwa na Creative Associates International.Yaliyomo katika kitabu hiki yanatokana na mwandishi na mchapishaji wake na hayawakilishi maoni na msimamo wa USAID wala Serikali ya Marekani.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri,kupiga chapa kitabu hiki au sehemu yake kwa njia yoyote ile bila ya idhini ya 21st Century Basic Education Program(TZ21).

Mti huu wa ajabu, watu wanaustaajabu.
Una mambo ya ajabu, toka enzi za mababu.
Mti huu mti gani?



Mti wake wa ajabu, mimi hunipa taabu.
Magamba yake ya ajabu, sote twastaajabu.
Mti huu mti gani?

Majani yake ya kijani, yanawiri bila kifani.
Umejaa mashambani, mjini na vijijini.
Mti huu mti gani?





Nikiuona natamani, na wala siyo utani.
Kuuchimba natamani, niutoe magambani.
Mti huu mti gani?

Ukiwekwa hadharani, watu wanautamani.
Mti wake na majani, kuuacha hutamani.
Mti huu mti gani?

Na wanyama hutamani, kuyala yake majani.
Na wengine masikini, mizizi huitamani.
Mti huu mti gani?



Tena uwe makini, uchimbapo ardhini.
Usipokuwa makini, utautia hatarini.
Mti huu mti gani?

Mlo wake ni makini, asubuhi hata jioni.
Waleta shibe tumboni, na hata nguvu mwilini.
Mti huu mti gani?

Mboga yatokana na majani, ugali, keki mizizini.
Shina kwa mbegu na kuni, vijijini hata mjini.
Mti huu mti gani?



Maajabu yamkini, kwa tajiri na maskini.
Kila kitu ni thamani, mti huu mti gani?
Jibu muhogo jamani!

Maswali ya Ufahamu

1. Kwa nini mti huu ni wa ajabu?
2. Mti wa ajabu unafaa kwa mambo gani?
3. Unadhani zao gani lililochimbwa ardhini?
4. Taja faida za mti huo.

Msamiati

Eleza maana ya maneno haya:

1. Maajabu
2. Magamba
3. Nawiri
4. Tamani
5. Shibe

Jaza herufi zinazokosekana katika maneno haya:

1. Staaj _bu
2. _ifani
3. M_zi_ _
4. M_h_go
5. M_kin_